

BARAZA LA TAIFA LA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI



TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 23 Juni 2016 lilipitisha mswada wa sheria ya Fedha ya mwaka 2016 (yaani The Finance Act, 2016) ambao pamoja na mambo mengine ulifanyia mabadiliko sheria ya eletroniki na mawasiliano ya posta (yaani Electronic and Postal Communications Act, Cap 306) yenye lengo la kuyataka makampuni ya mawasiliano yaliyoandikishwa kufanya biashara hapa nchini kumilikisha asilimia 25 ya hisa zake kwa umma kwa kujiunga na soko la hisa la Dar es Salaam ndani ya kipindi cha miezi 6 kuanzia tarehe 1 Julai 2016.

Mabadiliko haya ya kisheria katika sekta ya mawasiliano nchini inayojumuisha makampuni ya simu za mikononi yana lengo la kuongeza uwazi katika usimamizi wa makampuni haya na kuongeza makusanyo ya kodi zaidi kwa serikali. Pia mabadiliko haya yanatoa fursa ya kuwawezesha watazania kiuchumi kwa kuwa wamiliki wa makampuni haya kupitia ununuaji wa hisa katika soko la hisa la Dar es Salaam. Zaidi ya Watanzania milioni 20 wanamiliki na kutumia simu za mikononi katika shughuli zao za kila siku.

Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi linatoa rai kwa makampuni ya simu za mikononi (Mobile Telecommunications Companies) hapa nchini kutekeleza mabadiliko haya ya kisheria ndani ya muda uliotolewa kwa kukamilisha taratibu za kisheria za masoko ya mitaji na hisa kwa kutoa asimilia 25 ya hisa zao na kujiunga na soko la hisa la Dar es Salaam ili kuwezesha wananchi kununua hisa hizo na kuwa sehemu ya wamiliki wa kampuni hizi hapa nchini.

Aidha, Baraza linatoa wito kwa watazania wote kujiandaa kushiriki kikamilifu katika kununua hisa za makampuni haya ya simu mara yatakapokamilisha taratibu za kujiunga na soko la hisa la Dar Es Salaam. Baraza litatoa elimu kwa umma kwa muda mwezi mmoja kuanzia sasa kupitia vyombo vya habari kama vile Magazeti, Radio na

Televisheni katika kuelimisha na kuhamasisha umma kuhusu fursa hii muhimu kiuchumi. Elimu itatolewa kwa umma kuhusu namna ya kushiriki kununua hisa, faida za kununua hisa pamoja na athari zake.

Kuna faida nyingi sana kiuchumi kama watazania watashiriki kikamilifu kwenye ununuzi wa hisa kwenye makampuni ya simu nchini. Mtanzania atanufaika na faida hizi kama ifuatavyo:

1. Kumiliki kampuni za simu za mikononi.
2. Kupata gawio la faida kutoka kwenye kampuni.
3. Kupata faida wakati thamani ya hisa ikiongezeka.
4. Kupata upendeleo wa hisa za ziada wakati kampuni ikiamua kutoa hisa.
5. Kutumia hisa kama dhamana ukitaka mkopo benki.
6. Hisa ni pesa mara moja.

Pia Baraza linatoa rai kwa Mashirika ya Hifadhi ya Jamii Nchini kuandaa utaratibu mzuri utakaowawezesha wanachama wao kuweza kushiriki katika kununua hisa za makampuni haya ya simu mara yatakapojiunga na soko la hisa.

Baraza la Taifa la Uwezeshaji litafuatilia kwa karibu maendeleo ya utekelezaji wa mabadiliko haya ya kisheria na kuhakikisha utekelezaji wake unafanyika kwa wakati kama ilivyoainishwa katika sheria ya fedha ya mwaka 2016.

Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) lilianzishwa kupitia Sheria ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, namba 16 ya mwaka 2004, kama chombo cha juu cha kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi lipo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na linasimamia Mkakati wa Kitaifa wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kupitia madawati ya uwezeshaji kuanzia ngazi ya Wizara, Idara, Taasisi, Mikoa na Halmashauri zote nchini.

Imetolewa na,

Beng'i Issa

Katibu Mtendaji

Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

Dar es Salaam,

21 Novemba, 2016

